


MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2024 KWA MKOA WA KUSINI, UNGUJA Umetolewa: 22/02/2024

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi - Mei, 2024; athari na ushauri kwa sekta mbalimbali katika mkoa wa Kusini, Unguja na wilaya zake:

(I) Ngazi ya Mkoa



Kielelezo 1: (a) Mwelekeo wa msimu wa Masika, 2024 kwa mkoa wa Kusini, Unguja. (b) Ramani inayoonesha wastani wa muda mrefu wa mvua za msimu wa Masika katika sehemu mbalimbali za mkoa wa Kusini, Unguja. **Angalizo:** Wastani wa muda mrefu (miaka 30) wa mvua za mwezi Machi hadi Mei, mabadiliko ya mvua kati ya mwaka mmoja na mwingine yamezingatiwa.

Dondoo

- Hali ya El Niño inayoendelea kwa sasa katika Bahari ya Pasifiki inatarajiwa kupungua nguvu hususan tunapoelekea katika msimu wa mvua za Masika, 2024.
- Kwa ujumla mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya mkoa wa Kusini, Unguja.
- Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari, 2024.
- Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.
- Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2024.

Mvua za msimu wa Masika, 2024

Kwa ujumla mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani katika maeneo mengi ya wilaya za mkoa wa Kusini, Unguja.

Angalizo:


Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza katika msimu huu wa Masika, 2024

Utubiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2024 KWA WILAYA YA KUSINI Umetolewa: 22/02/2024

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2024; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kusini.

 <p>Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi-Mei), 2024 kwa wilaya ya Kusini, Unguja.</p>	<h3>Dondoo muhimu</h3> <ol style="list-style-type: none">Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kusini.Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari 2024.Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.
--	---

<h3>Mvua za msimu wa Masika, 2024 kwa wilaya ya Kusini</h3> <p>Zitaanza: Wiki ya nne ya Februari, 2024.</p> <p>Zitaisha: Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.</p> <p>Kiasi cha mvua zinazotarajiwa: Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Kusini ni kati ya milimita 490 hadi 680.</p> <p>Kiwango cha juu cha mvua: Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2024.</p> <p>Vipindi vya ukavu: Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2024.</p> <p>Ulinganifu: Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.</p> <p>Angalizo:</p> <ul style="list-style-type: none">Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa.Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.


<h3>Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi</h3> <h4>Matokeo</h4> <ol style="list-style-type: none">Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza.Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo.Upatikanaji wa chakula kwa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha. <h4>Ushauri</h4> <ol style="list-style-type: none">Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.Wakulima wa mwani wanashauriwa kulima mwani kwenye maji ya kina kirefu ili kuondokana na athari za maji ya mvua yanayokuwa yanaingia baharini.Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa.Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae.Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya baharini yakiwemo maghala ya baridi.
--

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz

(II) Ngazi ya Wilaya

MWELEKEO WA MVUA ZA MASIKA (MACHI – MEI), 2024 KWA WILAYA YA KATI Umetolewa: 22/02/2024

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa mvua za Masika katika kipindi cha Machi-Mei, 2024; athari na ushauri kwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi katika wilaya ya Kati

 <p>Mwelekeo wa mvua za Masika (Machi-Mei), 2024 kwa wilaya ya Kati Unguja.</p>	<p>Dondoo muhimu</p> <ol style="list-style-type: none"> Mvua za Wastani hadi Juu ya Wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya wilaya ya Kati. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya nne ya mwezi Februari 2024. Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024. Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi.
---	---

<p>Mvua za msimu wa Masika, 2024 kwa wilaya ya Kati</p> <p>Zitaanza: Wiki ya nne ya Februari, 2024.</p> <p>Zitaisha: Kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.</p> <p>Kiasi cha mvua zinazotarajiwa: Mvua zinatarajiwa kuwa za Wastani hadi Juu ya Wastani. Kwa kawaida wastani wa mvua katika miezi ya Machi-Mei kwa wilaya ya Kati ni kati ya milimita 490 hadi 850.</p> <p>Kiwango cha juu cha mvua: Kinatarajiwa katika mwezi Machi, 2024.</p> <p>Vipindi vya ukavu: Upo uwezekano wa kutokea vipindi vya ukavu vya siku kumi (10) au zaidi katika msimu huu wa Masika, 2024.</p> <p>Ulinganifu: Mvua zinatarajiwa kuwa nyingi na zenye mtawanyiko mzuri katika maeneo mengi ukilinganisha na Masika iliyopita.</p> <p>Angalizo:</p> <ul style="list-style-type: none"> Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya taarifa za utabiri wa hali ya hewa. Watumiaji wa taarifa hii wanashauriwa kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10, mwezi pamoja na tahadhari kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. 	<p>Matokeo na ushauri kwa kilimo, mifugo na uvuvi</p> <p>Matokeo</p> <ol style="list-style-type: none"> Wadudu waharibifu na mlipuko wa magonjwa ya mifugo na mazao yanayoambatana na mvua nyingi yanaweza kujitokeza. Vipindi vya unyevu wa kuzidi kiasi pamoja na mafuriko vinaweza kujitokeza na kuathiri mazao pamoja na miundombinu ya kilimo. Upatikanaji wa chakula kwa mazao ya baharini unatarajiwa kuwa wa kuridhisha. <p>Ushauri</p> <ol style="list-style-type: none"> Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba, kupanda, kupalilia na kutumia pembejeo husika kwa wakati na kuchagua mbegu na mazao sahihi. Wakulima wa mwani wanashauriwa kulima mwani kwenye maji ya kina kirefu ili kuondokana na athari za maji ya mvua yanayokuwa yanaingia baharini. Matumizi sahihi ya mbinu bora na teknolojia za kuzuia maji shambani, mmomonyoko na upotevu wa rutuba, vinashauriwa. Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu bora za ufugaji ili kutunza malisho na kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadae. Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya baharini yakiwemo maghala ya baridi.
---	---

Utabiri wa hali ya hewa nchini na tahadhari zinapatikana katika tovuti ya Mamlaka: www.meteo.go.tz